- Circuler pour écouter les élèves lire et les aider au besoin.
- Après 2 minutes, demander aux autres de lire

#### b. Lecture individuelle du texte à haute voix (10 min)

**M :** Sasa wanafunzi tatu wasome moja kwa moja kwa sauti kubwa. Wengine wasome na sauti ya cini kiisha watie kidole kwenyi maneno wanayo soma.

- Circuler et demander à 7 élèves de pointer les mots qui sont en train d'être lus.

#### Mafaa ya pori

Leila na Davido wanaenda kulunguza pori. Wanabebea **kibiriti**. Njia ni **nyembamba** na miti ni mirefu. **Matawi** ni mengi na yenyi kukauka. Wanasiakia **mlio** neuri wa ndege, wa wanyama na vidudu vya kila aina.

Davido akasema: «Tukiunguza pori, miti itaunga na wandege watafariki.»

Leila anasema : «Pori yatupatia cakula. Wanyama ni mali ya inci yetu.»

#### c. Compréhension du vocabulaire (5 min)

**M :** Njia ya pori iko namna gani ? (Iko nyembamba)

**M :** **Nyembamba** ni mtu ao kitu yenyi mwili ndogo. Kwa mfano: Kijana huyu ana mwili mwembamba.

**M :** Nyinyi pia, Mutunge misemwa inayo neno « **Nyembamba** »

**M:** Pori yatupatia nini? (Cakula)

- Suivre la même démarche avec le mot : **Matawi, mlion, kibiriti...**

#### d. Compréhension du texte (10 min)

- Faire réfléchir en paire / pupitre,
- Confronter les réponses et demander des justifications

**M :** Wanani wanapita katika pori ? (Leila na Davido.)

**M :** Njia ya pori iko namna gani ? (ni nyembamba.)

**M :** Sababu gani Leila na Davido walibeba kibiriti ?

(Sababu walunguze pori)

**M :** Leila na Davido, waliluguza tena pori? Sababu gani? Reponses libres

**M :** Unawaza wazo ya kulunguza porini nzuri? Sababu gani? Reponses libres

**Faire réfléchir en paire / banc, confronter les réponses et demander des justifications**

## C. ACTIVITES DE CONTROLE

### 3. Evaluation (5 min)

#### a. Lecture des phrases du texte

- Choisir 7 à 10 élèves pour lire à haute voix des phrases du texte dans leur manuel. Noter et aider ceux qui ont des difficultés.

**M :** Someni ndani ya buku zenu kwa sauti ya juu misemwa yenyi nitasema.

#### b. Compréhension

**M :** Hadisi yetu ilizungumuza kuhusu nini ?

**M :** Nitataja misemwa. Kama msemwa ni sawa, muinue kidole gumba. Kama si sawa, mutie mikono uu ya marfaa.

**M :** Leila na Davido walipita porini. ↗

**M :** Leila na Davido waliluguza pori. (--) ↗

**M :** Pori yaleta cakula na mali ya inci ↗

**M :** Andika ndani ya buku yako majina ya miti mbalimbali.

#### Devoir à domicile

**M :** Wanafunzi wapenzi, nyumbani, musomee wazazi wenu usomi wa leo kwenyi ukurasa wa 39. Kiisha, muandike misemwa kuhusu mimea mbalimbali.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N° 10

### LEÇON N° 10.3

Thème: La flore

Sous-thème : Végétation - La cœullette

**Sujet de la leçon:** Mafaa ya pori

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d'):

- relire avec expressivité le texte gradué;
- utiliser les classes nominales **mu/mi** à l'oral et à l'écrit

**Matériel didactique:** Texte du Manuel de l'élève

**Références:** Guide de l'enseignant ;  
Manuel de l'élève, p. 39-40

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Rappel des idées importantes du texte (5 min)

**M :** Hadisi gani tulijifunza jana ? Mafaa ya pori

**M :** Wawili wawili mujibu ku maulizo.

**M :** Leila na Davido walienda wapi ?

**M :** Mawazo gani Davido alipata ?

- Choisir 2 à 3 élèves pour répondre à chaque question.

#### B. ACTIVITES PRINCIPALES

##### 2. Relecture du texte en paire à voix basse (15 min)

**M :** Mufungue vitabu vyenu ku ukurasa wa 39.

**M :** Someni hadisi « **Mafaa ya pori.** » Wawili wawili kwa marfaa. Mmoja asome mwenzake afwate. Yule anafanya makosa, mwenzake amusahihishe.

**M :** Wale wanataka kusoma mbele wainue kidole.

**M :** Someni tangu mwanzo wa hadisi mpaka mwisho.

- Circuler pour écouter les élèves lire et les aider au besoin.
- Après 2 minutes, demander aux autres de lire.

#### 3. Grammaire (20 min)

##### a. Appropriation des emplois de la règle: la classe nominale mu/mi (5 min)

**M :** Someni msemwa huu : **Njia ni nyembamba na miti ni mirefu.**

**M :** Kitu gani iko murefu ? **Mti.**

**M :** Neno **mti** ni ku umoja. Ku uwingi ni **miti**.

**M :** “Idadi umoja wa majina inayo tamko **mu** inabeba tamko **mi** ku idadi uwingi.”

Kwa mfano: **muhogo-mihogo, murefu-mirefu, muguu- miguu, muhindi-mihindi**

- Penser à faire répéter.

##### b. Production de phrases avec les classes nominales (5 min)

**M :** Kila mwanafunzi atunge misemwa munamo idadi umoja na tamko **mu** na idadi uwingi na tamko **mi** kiisha muandike ndani ya buku zenu.

**M :** Wanafunzi wane wapite mbele waandike misemwa yao ku ubao.

- Interroger 2 à 3 élèves qui écrivent au tableau leur phrase. Faire appel aux autres élèves pour corriger.

#### C. ACTIVITES DE CONTROLE

##### 4. Evaluation (5 min)

**M :** Taja majina mbalimbali zinazo tamko **mu** uitie ku uwingi iwe na tamko **mi**.

**M :** Kila mmoja aandike maneno munamo aina ya majina mu -mi ndani ya buku lake.

- Après 3 minutes, interroger 5 élèves pour qu'ils lisent leur propre phrase.

#### Devoir à Domicile

**M :** Wanafunzi wapenzi, nyumbani, andikeni majina kwa uwingi na kwa umoja, kwenyi ukurasa wa 40.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N°10

### LEÇON N° 10.4

Thème: La flore

Sous-thème : Végétation - La cueillette

**Sujet de la leçon:** Les textes de la semaine

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d'):

- lire avec expressivité le texte gradué
- employer les mots de vocabulaire ciblés
- construire une phrase à l'oral et à l'écrit à partir d'une consigne

**Matériel didactique:** Image du manuel de l'élève...

**Références:** Guide de l'enseignant ;  
Manuel de l'élève, p. 39 et 41

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Consolidation (15 min)

**M :** Sasa, tutasoma hadisi yeniyi tulijifunza wakati uliyopita.

**M :** Fungueni vitabu vyenu kwenyi ukurasa wa 39. kiisha someni hadisi « **Mafaa ya pori** » na sauti ya juu.

#### B. ACTIVITES PRINCIPALES

##### 2. Production orale (10 min)

###### a. Rappel du thème / sous-thème (5 min)

**M :** Juma hii mzima tulisemelea kuhusu nini ?

**M :** Maneno gani mapya tulijifunza tokeya hadisi yetu kuhusu Mti wa avokati ?

###### b. Construction de phrases (5 min)

- Faire construire oralement des phrases ; en retenir une et montrer la structure de cette phrase.

**M :** Tunacagua msemwa huu : « Helena alipanda mti wa avokati. »

**M :** Helena alipandanini ? **Mti**.

**M :** Ni kitu gani weye utafanya kwa kukinga mazingira ?

**M :** Kila wakati mbele ya kujibu aanza msemwa wako hivi : « **Kwa kukinga mazingira nita...** » kiisha oungeze wazo lolote unataka.

**M :** Sasa, mutaje vitu mbalimbali mutafanya kwa kukinga mazingira.

- Ecrire au tableau les mots intéressants liés au thème que les élèves ont trouvés et compléter éventuellement la liste.

#### 3. Production écrite (15 min)

- Donner une consigne et former des groupes de 4 élèves / 2 bancs

**M :** Sasa, Mtumike katika kundi ya wanafunzi wane wane kwa kila marfaa, muandike kitu moja wala mbili mutafanya kwa kukinga mazingira.

**M :** Mukumbuke kuanza msemwa wenu hivi: **Kwa kukinga mazingira, tunapenda .....**

**Kiisha muongeze maneno yeniyi patikana ku ubao:** (lima, kuvuna, kupanda miti..)

- Attendre 5 minutes et envoyer, au tableau, 3 élèves pour écrire leur phrase.

**M :** Sasa kiongozi wa kila kundi apite ku ubao aandike msemwa yenye waliandika katika kundi lao.

**M :** Tazameni vizuri ginsi mwenzenu anaandika, kama anafanya makosa musahihishe.

#### C. ACTIVITES DE CONTROLE

##### 4. Evaluation (5 min)

**M :** Sasa, kila mmoja akamate buku yake aandike ile atafanya kwa kukinga mazingira.

**M :** Kumbuku kuanza msemwa wako na: « **Kwa kukinga mazingira nita...** » kiisha andika ile utafanya kwa kukinga mazingira.

##### Devoir à domicile

**M :** Wanafunzi wapenzi nyumbani cagua maneno isiyo angalia mimea na mavuno, jaza msemwa , kiisha, andika misemwa kuhusu mimea na mavuno.

##### Auto évaluation de l'enseignant:

Pour chaque activité dans cette leçon, comptez les élèves dans votre classe qui ont maîtrisé et pu faire cette activité. Si 50% ou plus de vos élèves n'ont pas pu faire une activité ou plusieurs des ACTIVITES, référez-vous au tableau « ACTIVITES de remédiation » à l'annexe de ce guide. Mener cette/ces activité(s) avec vos élèves avant d'avancer à la prochaine unité.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N° 11

### LEÇON N° 11.1

Thème : La flore

Sous-thème : Sauvegarder l'environnement

#### Sujet de la leçon: Mtu na mazingira

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d'):

- utiliser les mots du vocabulaire ciblés liés au thème
- répondre aux questions de compréhension du texte


**Matériel didactique:** Affiche n°11

**Références :** Guide de l'enseignant ; Manuel de l'élève, p. 42

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Observation et exploitation de l'image (10 min)

- Pointer l'image de l'affiche.



**M :** Tazameni vizuri sanamu hii,

**M :** Wawili wawili, wala kwa marfaa, kila mmoja aambie mwenzake ile anaona kwenyi sanamu.

**M :** Huyu baba iko anafanya nini ?

**M :** watu hawa wakonafanya nini?

**M :** Munawaza hadisi yetu itazungumuzia kuhusu nini?

- Demander aux élèves de réfléchir par banc ; en choisir 2 à 3 pour répondre ; Apprécier les réponses différentes.

**M :** Sasa tutasoma, ili tupate kujua nini itapita.

#### B. ACTIVITES PRINCIPALES

##### 2. Etude du texte (25 min)

###### a. Lecture du texte à haute voix (5 min)

**M :** Mufwate hadisi hii vizuri. Kiisha mutajibu ku maulizo..

###### Mtu na mazingira

Nilazima Mtu kukinga **mazingira**. Kijiji moja, ilikuwa na watu wengi. Kandokando yake, kulikuwa miti mirefu, mto na **kisima**. Maisha ilikuwa nzuri sana.

Wakati moja wamama wakaanza kutupa uchafu ndani ya mto.

Wababa nao wakaanza kukata miti sana na kucoma pori. Bahada ya vitendo hivi, vinyume vikajitokeza. watu wakaanza kugonjwa kwa kunywa na kujiosha kwa maji cafu.

Kijiji haikuwa tena na **kinvuli**. **Joto** ikawa mungi sana. Udongo ukakauka, ukakosa mboleo, kisima haitowe tena maji. Samaki ikafa, mimea ikakauka. Wakaaji wakaaca kijiji cao, wakaenda ugeni mji wa **kandokando**.

Wakaaji wa Kijiji hico wakawatesa sana. Hawakuwapa maji, cakula hata fasi ya kulala. Kiisha siku cace, **wakaamua** warudi kwao. Wakapanda miti, kinvuli ikarudi, kisima ikatoa maji, Maisha ikarudi nzuri. Tukinge mazingira yetu, ili, tusikose cakula, maji na hewa nzuri.

###### b. Compréhension du vocabulaire (5 min)

**M :** Nilazima Mtu kukinga nini ? (**Mazingira**)

**M :** **Mazingira** ni vitu vinavyo kuwa kandokando ya mtu na kwa mafaa yake. mfano: pori, mito, udongo, ...

**M :** Sikilizeni msewma munamo neno **mazingira**. Mfano: Tupande miti kwa kukinga **mazingira**.

**M :** Sasa nanyi vilevile mutunge misewa munamo neno "**Mazingira**"

- Suggérer les situations de communication au besoin.
- Faire la même chose avec les mots : **Kisima**, **Kinvuli**, **kandokando**, **wakaamua**.

###### c. Compréhension du texte (15 min)

- Relire le texte une fois et procéder par le questionnement par paire / banc.
- Apprécier les réponses et demander des justifications.

**M :** Fwateni vizuri nitasoma tena hadisi yetu, badae, mutajibu ku maulizo.

**M :** Kijiji hiki kilikuwa na wanani ? (**Kilikuwa na watu wengi**)

**M :** Nini ilikuwa kandokando ya kijiji ? (**Mto**, **miti mirefu**, **na Kisima**)

**M** : watu walikata miti sababu ya nini ? (**Kufanya kuni, makaa, mbao, kujengea nyumba**)

**M** : Kiisha kukata miti ya kijiji, vinyume gani ilifika ? (**Kijiji haikuwa tena na kinvuli. Joto ikahawa mingi sana. udongo ukakauaka mboleo, kisima haitowe tena maji. samaki wakafa, Mimea ikakauka.**)

**M** : Wakaaji wa kijiji walifanya nini ? (Wakaaji wakaaca kijiji cao, wakaenda ugeni mji wa kandokando.)

**M** : Wewe mitendo gani nzuri umefanya kwa kulinda mazingira ya Kijiji kyenu? (**Réponse libre**)

### C. ACTIVITES DE CONTROLE

#### 3. Evaluation (10 min)

##### a. Compréhension

**M** : Nitasema kuhusu hadisi yetu. Kama msemwa ni kweli, uinue kidole gumba. Kama msemwa si sawa, utie mkono juu ya marfaa.

**M** : Hadisi inasemea kuhusu kukinga mazingira. ☺

**M** : Kukata miti ovyo ni kukinga mazingira. (--)

**M** : Kiisha ya kutata miti joto ikahawa mingi. ☺

**M** : wakaaji wa kijiji ya kandokando waliwapokea vizuri. (--)

**M** : Andika kwa misemwa mbili, matendo unafanya kwa kukinga mazingira yako.

##### b. Vocabulaire

**M** : Nitasema misemwa. Kama msemwa ni sawa, uinue kidole gumba. Kama msemwa si sawa, mutie kidole juu marfaa.

**M** : Mazingira ni vitu vinavyo tuzunguuka na kufaa kwa maisha yetu. ☺

**M** : Kinvuli ni joto (--)

**M** : Kisima ni nafasi ya kucota maji ya kunya ☺

**M** : Kandokando ni mbali nasi (--)

##### Devoir à domicile

**M** : Wanafunzi wapenzi, nyumbani, muelezee wazazi na wandugu wenu hadisi ya leo. Kiisha andikeni matendo mutafanya kwa kukinga mazingira, kwenyi ukurasa wa 42.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N° 11

### LEÇON N° 11.2

#### Thème: La flore

#### Sous-thème : Sauvegarder l'environnement

**Sujet de la leçon:** Tuheshimu mto

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d'):

- lire avec expressivité le texte gradué
- employer les mots de vocabulaire ciblés
- répondre aux questions de compréhension sur le texte

**Matériel didactique:** Image du manuel de l'élève...

**Références:** Guide de l'enseignant ; Manuel de l'élève, p.43

### A. ACTIVITES INITIALES

#### 1. Observation et exploitation de l'image (5 min)

**M** : Mufungue vitabu vyenu ku ukurasa wa 43.

**M** : Tazameni sanamu hii.

**M** : Munaona nini ?

**M** : Watoto hawa wako wapi ?

**M** : Wanafanya nini ?

**M** : Kutokea sanamu hii, munawazia hadisi ya leo itasemelea nini ?

- Demander aux élèves de réfléchir en paire / banc ; en choisir 3 à 4 pour répondre ; Apprécier les réponses différentes ; corriger et renforcer les réponses.



## B. ACTIVITES PRINCIPALES

### 2. Etude du texte (35 min)

#### a. Lecture du texte en paire à voix basse (10 min)

**M :** Tazameni usomi hii. Ina vipindi ngapi? Kipindi ya kwanza inaanza na neno gani, inaishia inaisha na neno gani?

**M :** Wawili wawili wala kwa marfaa, musome mmoja Kiisha mwengine. Anae magumu, mwenzake amusahihishe.

**M :** Yule atakaesoma wa kwanza ainue kidole na asome kwa sauti ya cini.

- Circuler pour écouter les élèves lire et les aider au besoin.
- Après 2 minutes, demander aux autres de lire

#### b. Lecture individuelle du texte à haute voix (10 min)

**M :** Sasa wanafunzi tatu wasome kwa sauti ya juu, mmoja Kiisha mwengine, na wale wanataka kusoma wasome kwa sauti ya cini, wakiweka kidole kwa kila neno wanasoma.

- Circuler, faire pointer les mots et changer quelquefois l'ordre des phrases.

#### Tuheshimu mto

Mto ni yenyi **mafaa** kwetu. Inasaidia watu, nyama pia mimea. Watu wanaishi kandokando ya mto. Wanajiosha na kuivisha cakula kwa maji yake.

**Kucafua** mto imekatazwa. Tukumbuke watu wanaishi cini ya mto. Samaki pia **wanahitaji** maji safi.

#### c. Compréhension du vocabulaire (5 minute)

**M :** Mto ni yenyi nini kwetu ? mafaa.

**M :** Mafaa ni kitu yenyi faida.

**M :** Sikilizeni msempa yenyi neno mafaa: Kujua kusoma ni yenyi mafaa kwa mtu.

**M :** Sasa kila mmoja atunge msempa na neno **mafaa**.

- Suggérer des situations de communication, au besoin
- Faire de même avec **kucafua et wanahitaji**

#### d. Compréhension du texte (10 min)

**M :** Nini inasaidia watu, nyama na mimea? (Mto)

**M :** Watu wanafanya nini kandokando ya mto ? (Wanaishi)

**M :** Sababu gani kucafua mto imekatazwa ? (Watu ujiosha na kuivisha cakula kwa maji ya mto.)

**M :** Wanani pia wanahitaji maji safi? (Samaki)

**M :** Maji ya mto ikiwa cafu inaweza kulete vinyume gani ? (Réponse libre)

- Faire réfléchir en paire / banc, confronter les réponses et demander des justifications

## C. ACTIVITES DE CONTROLE

### 3. Evaluation (5 min)

#### Lecture des phrases du texte

- Choisir 7 à 10 élèves pour lire à haute voix des phrases du texte dans leur manuel. Noter et aider ceux qui ont des difficultés.

**M :** Someni kwa sauti ya juu misemwa ya usomi nitakayoonesha ndani ya vitabu vyenu.

#### b. Compréhension

**M :** Usomi wetu wa leo unasemea kuhusu nini ? (Tuheshimu mto)

**M :** Sasa nitasema misemwa, kama ni kweli, inua kidole gumba, kama si kweli, tia mikono juu ya marfaa.

**M :** Mto ni yenyi mafaa kwetu ➤

**M :** Mto haifae kwa mimea (–)

**M :** Kucafua mto imekatazwa ➤

**M :** Samaki wanahitaji maji cafu (–)

**M :** Andika ndani ya buku yako majina ya nyama za pori.

#### Devoir à domicile

**M :** Wanafunzi wapenzi, nyumbani, musomée wazazi wenu usomi wa leo kwenyi ukurasa wa 43.

**Kiisha muandike** ndani ya buku yenu msempa kuhusu kuingira.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N° 11

### LEÇON N° 11.3

Thème: La flore

Sous-thème : Sauvegarder l'environnement

#### Sujet de la leçon: Tuheshimu mto

Objectifs: L'élève sera capable de (d'):

#### relire avec expressivité le texte gradué

- identifier les mots qui peuvent occuper la fonction du sujet dans une phrase à l'oral et à l'écrit

Matériel didactique: Texte du Manuel de l'élève...

Références: Guide de l'enseignant ; Manuel de l'élève, p. 43-44

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Rappel des idées importantes du texte (5 min)

M : Usomi yetu ya jana ilisema kuhusu nini ? (Tuheshimu mto).

M : Nini inasaidia watu, nyama na mimea ?(Mto)

M : watu wanafanya nini kandokando ya mto ?(Wanaishi)

M : Sababu gani kucafua mto imekatazwa ? (Watu ujiosha na kuivisha cakukula kwa maji ya mto)

M : Wanani pia wanahitaji maji safi? (Samaki)

- Choisir 2 à 3 élèves pour répondre à chaque question.

#### B. ACTIVITES PRINCIPALES

##### 2. Relecture du texte en paire à voix basse (15 min)

M : Mufungue vitabu vyenu kwa ukurasa wa 43.

M : Msome tena hadisi « Tuheshimu mto » na mwenzako wa marfaa, mmoja Kiisha mwengine. Mwenzako akimagumu, umusahihishe.

Wale wanaohitaji kusoma wainuwe mbele kidole.

M : Someni kwanza na sauti ya cini mpaka mwisho. Mukibadilisha zamu, mmoja asome, na mwengine amusikilize na kusahihishe.

- Circuler pour écouter les élèves lire et les aider au besoin.
- Après 2 minutes, demander aux autres de lire.

#### 3. Grammaire (20 min)

##### a. Appropriation des emplois de la règle: la fonction du sujet (10 min)

M : Someni msemwa huu : **Mto ni yenyé mafaa kwetu.**

M : Msemwa wetu unaanza na neno gani ? (**Mto**)  
**Sikilizeni namna ninavyo uliza kwa kupata neno "mto"**

M : Nini yenyé mafaa kwetu ? (**Mto**)

M : Neno mto linajulisha nini ? **Mtendaji.** Basi namna gani tunaita mtendaji ? (Mwenyi wa tendo)

« Mwenyi wa tendo ni neno lenyi kujulisha mwenyi kutenda. »

Kwa kupata mwenyi wa tendo ndani ya msemwa, tunatumia ulizo « nani ao nini » mbele ya tendo. »

M : Tusome tena msemwa wa pili ndani ya hadisi. Inasaidia watu, nyama pia mimea.

Ntamko "I" mbele ya neno saidia ina wakilisha neno mto.

"Basi kazi ya mwenyi wa tendo inaweza pia kufanyika na **kiwakilishi** ao **tendo** lenyewe".

Mfano wa kiwakilishi kuwa mweyi wa tendo:

M : Tusome msemwa wa tatu:

Nini imekatazwa? (**Kucafua**). **Kucafua** ni nini? (**Tendo**).

“**Tendo** ni neno lenyi kuonyesha kazi inayotendeka.”

- Penser à faire répéter.

##### b. Production de phrases avec le sujet (10 min)

M : Kila mwanafunzi atunge misemwa munamo mwenyi wa tendo ni jina, kiwakilisha ao tendo lenyewe kiisha muaandike ndani ya buku zenu.

M : Wanafunzi wane wapite mbele waandike misemwa yao ku ubao.

- Interroger 2 à 3 élèves qui écrivent au tableau leur phrase. Faire appel aux autres élèves pour corriger.

#### C. ACTIVITES DE CONTROLE

##### 4. Evaluation (5 min)

M : Sasa, kila mmoja atunge misemwa mbili, na atie kistari cini ya neno msingi.

- Après 3 minutes, interroger 5 élèves pour qu'ils lisent leur propre phrase.

#### Devoir à Domicile

M : Nyumbani cagua misemwa yenyi kuwa na mwenyi wa tendo ndani ya usomi wetu. Kiisha, andika misemwa yenyi mwenyi wa tendo, kwenyi ukurasa wa 44.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N°11

### LEÇON N° 11.4

**Thème:** La flore

**Sous-thème :** sauvegarder l'environnement

**Sujet de la leçon:** Les textes de la semaine

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d'):

- lire avec expressivité le texte gradué
- employer les mots de vocabulaire ciblés
- identifier les mots qui peuvent occuper la fonction du sujet dans une phrase à l'oral et à l'écrit

**Matériel didactique:** Image du manuel de l'élève...

**Références:** Guide de l'enseignant ; Manuel de l'élève, p. 43 et 45

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Consolidation (15 min)

**M :** Sasa, tutasoma hadisi yenyi tulijifunza wakati uliyo pita

**M :** Fungueni vitabu vyenu kwenyi ukurasa wa 43. Kiisha someni hadisi « Tuheshimu mto » na sauti ya jjuu.

#### B. ACTIVITES PRINCIPALES

##### 2. Production orale (10 min)

###### a. Rappel du thème / sous-thème (5 min)

**M :** Juma hii mzima tulisemelea kuhusu nini ? (**Mtu na mazingira**)

**M :** Maneno gani mapya tulijifunza tokeya hadisi yetu kuhusu «Mtu na mazingira.»

###### b. Construction de phrases (5 min)

- Faire construire oralement des phrases ; ayant le nom, l'infinitif ou le pronom comme sujet, faire poser la question pour trouver le sujet.

**M :** Mutunge msemwa ambao "mwenye wa tendo" ni jina, tendo ao kiwakilisho

**M :** Tunacagua msemwa: « **Watu wanaishi kandokando ya mto.**»

**M :** Neno « **watu** » ni mwenye wa tendo.

**M :** Kila wakati mutapenda kutambua « mwenye wa tendo ndani ya msemwa » mutumiye ulizo « nani ao nini mbele ya tendo »

- Ecrire au tableau les phrases intéressantes liées au thème que les élèves ont construites

#### 3. Production écrite (15 min)

- Donner une consigne et former des groupes de 4 élèves / 2 bancs

**M :** Sasa, Mtumike katika kundi ya wanafunzi wane wane kwa kila marfaa, muandike misemwa na mupike kistari cini ya mwenye wa tendo.

**M :** Kwa kutambua mwenye wa tendo, Mukumbuke ulizo : nani ao nini mbele ya tendo.

- Attendre 5 minutes et envoyer, au tableau, 3 élèves pour écrire leur phrase.

**M :** Sasa kiongozi wa kila kundi apite ku ubao aandike msemwa yenyi waliandika katika kundi lao na kutia kistari cini ya mwenyi wa tendo.

**M :** Tazameni vizuri ginsi mwenzenu anaandika, kama anafanya makosa musahihishe.

#### C. ACTIVITES DE CONTROLE

##### 4. Evaluation (5 min)

**M :** Sasa, kila mmoja akamate buku yake aandike misemwa munamo mwenyi wa tendo ni jina ao kiwakilisha.

###### Devoir à domicile

**M :** Wanafunzi wapenzi nyumbani cagua jina isiyo angalia pori, jaza msemwa kissha, andika misemwa mbili kuhusu matendo unafanya kwa kukinga mazingira yako, kwenyi ukrasa wa 45.

###### Auto évaluation de l'enseignant:

Pour chaque activité dans cette leçon, comptez les élèves dans votre classe qui ont maîtrisé et pu faire cette activité. Si 50% ou plus de vos élèves n'ont pas pu faire une activité ou plusieurs des ACTIVITES, referez-vous au tableau « ACTIVITES de remédiation » à l'annexe de ce guide. Mener cette/ ces activité(s) avec vos élèves avant d'avancer à la prochaine unité.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N° 12

### LEÇON N° 12.1

Thème : Les animaux

Sous-thème : Les animaux domestiques

#### Sujet de la leçon: Imbwawa na Paka

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d') :

- utiliser les mots du vocabulaire ciblés liés au thème
- lire un texte avec expressivité ;
- répondre aux questions de compréhension du texte

**Matériel didactique:** Affiche n°12

**Références :** Guide de l'enseignant ;  
Manuel de l'élève, p. 46

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Observation et exploitation de l'image (10 min)

- Pointer l'image de l'affiche.



**M :** Tazameni vizuri sanamu hii.

**M :** Wawili wawili kwa marfaa, kila mmoja aambie mwenzake ile anaona kwenyi sanamu.

**M :** Wanyama wawili hawa ni nini ?

**M :** Wanyama hawa wako wapi ?

**M :** Mtu huyu anafanya nini katiki yao ?

**M :** Kiisha ya kutazama sanamu hizi, munazania hadisi yetu litasemea nini ?

- Demander aux élèves de réfléchir par banc ; en choisir 2 à 3 pour répondre ; Apprécier les réponses différentes.

**M :** Sasa tutasoma, ili tuvumbue hadisi yetu inasema kuhusu nini.

#### B. ACTIVITES PRINCIPALES

##### 2. Etude du texte (25 min)

###### a. Lecture du texte à haute voix (5 min)

**M :** Mufwate hadisi hii vizuri. Kiisha mutajibu ku maulizo..

###### Imbwawa na paka

Toka siku nyingi imbwawa na paka wako marafiki. Siku moja imbwawa anamuambia Paka : Jee, hauoni kama bwana wetu anatutesa ? Mimi, **ninakesha** kwa kokinga wezi hapa nyumbani, usiku kama vile mcana.

Wewe pia unafanya kazi kubwa. Unawinda panya nyumbani. Tazama, bwana wetu hatulipe hata kitu moja kwa kazi kubwa tunayo mufanyia ! Kwa hiyo, **ninaamua** kuondoka nyumbani na kwenda kuishi **porini**.

Wewe wahitaji kuja nami vilevile. Paka akamujibu : « Unaamua vizuri, lakini mimi ninafikiri kwa jambo moja : Tutajifica wapi wakati mvua itanyesha ? Ni **vema** wewe na mimi tuendelee kuishi na mtu.

Hata kama hatulipiwe kitu, lakini tunafaidika kwa kulishwa naye na kulala nyumbani mwake. Ndio maana imbwawa na paka wanaendelea kuishi na mtu pamoja.

###### b. Compréhension du vocabulaire (5 min)

**M :** Imbwawa anafanya nini kwa kokinga wezi nyumbani ? (**Anakesha**)

**M :** **Ninakesha** ni tendo Kukesha, Kukesha, ni kukaa bila kulala, ni kuangalia vizuri.

**M :** Sikilizeni msema munamo neno Kukesha: Zamu anakesha kwa kulinda mbuzi zetu.

**M :** Sasa nanyi vilevile mutunge misewa munamo neno "**kukesh**."

- Suggérer les situations de communication au besoin.
- Faire la même chose avec les mots : **ku amua, porini, vema**

###### c. Compréhension du texte (15 min)

- Relire le texte une fois et procéder par le questionnement par paire / banc.
- Apprécier les réponses et demander des justifications.

**M :** Fwateni vizuri nitasoma tena hadisi yetu, badae, mutajibu ku maulizo.

**M :** Toka siku nyingi imbwawa na paka wako wanani ? (**Marafika**)

**M :** Ibwa alikuwa na kazi gani nyumbani mwa mtu ? (Kukesha kwa kuinga wezi)

**M :** Kazi ya paka ilikuwa nayo gani ? (**Kuinda Panya**)

**M :** Sababu gani imbwa aliomba mwenzake waondoke nyumbani ? (kwani bwana wao hakuwalipa mshahara)

**M :** Kwa nini imbwa alikubali kuendelea kuishi pamoja na mtu? (**Réponses libres**)

**M :** Sasa wewe unafanya nini kwa kucunga na paka wenu? (**Réponses libres**)

### C. ACTIVITES DE CONTROLE

#### 3. Evaluation (10 min)

##### a. Compréhension

**M :** Nitasema kuhusu hadisi yetu. Kama msemwa ni kweli, uinue kidole gumba. Kama msemwa si sawa, utie kdole juu ya marfaa.

**M :** Imbwa na paka wako marafiki wa zamani. ☺

**M :** Imbwa alikuwa na kazi ya kuwinda panya (--)

**M :** Paka alimushauria imbwa aendelee kuishi nyumbani. ☺

**M :** Kwa mwisho waliondoka na kuishi porini. (--)

**M :** Andika kwa misemwa mbili, matendo unafanya kwa kucunga nyama za ufugo.

##### b. Vocabulaire

**M :** Nitasema misemwa. Kama msemwa ni sawa, uinue kidole gumba. Kama msemwa si sawa, utie kidole juu ya marfaa.

**M :** Kufungwa ni kuishi cini ya utawala ya mwengine. ☺

**M :** **Kuamua** ni kukataa (--)

**M :** **Kukesha** ni kukaa bila kulala kuangalia usiku nzima ☺

**M :** **Porini** ni juu ya mti. (--)

**M :** «**Vema**» ni kuitika ao kuhakikisha ☺

#### Devoir à domicile

**M :** Wanafunzi wapenzi, nyumbani, muelezee wazazi na wandugu wenu hadisi ya leo. Kiisha muandike majina za wanyama wa ufugo, kwenyi ukurasa wa 46.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N° 12

### LEÇON N° 12.2

#### Thème: Les animaux

#### Sous-thème : Les animaux domestiques

**Sujet de la leçon:** Paka yetu

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d'):

- lire avec expressivité le texte gradué
- employer les mots de vocabulaire ciblés
- répondre aux questions de compréhension sur le texte

**Matériel didactique:** Image du manuel de l'élève...

**Références:** Guide de l'enseignant ; Manuel de l'élève, p. 47

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Observation et exploitation de l'image (5 min)

**M :** Mufungue vitabu vyenu kwa ukurasa 47.


**M :** Tazameni sanamu hii.

**M :** Munaona nini?

**M :** Paka ikonafanya nini?

**M :** Kutokea sanamu hii, munawazia hadisi ya leo itasemea nini?

- Demander aux élèves de réfléchir en paire / banc ; en choisir 3 à 4 pour répondre ; Apprécier les réponses différentes ; corriger



ses.

#### B. ACTIVITES PRINCIPALES

##### 2. Etude du texte (35 min)

###### a. Lecture du texte en paire à voix basse (10 min)

**M :** Tazameni usomi hii. Ina vipindi ngapi? Kipindi ya kwanza inaanza na neno gani, inaishia inaisha na neno gani?

**M :** Wawili wawili wala kwa marfaa, musome mmoja kiisha mwengine. Anae magumu, mwenzake amusahihishe.

**M :** Yule anataka kusoma wa kwanza ainue kidole na asome kwa sauti ya cini.

- Circuler pour écouter les élèves lire et les aider au besoin.
- Après 2 minutes, demander aux autres de lire

### b. Lecture individuelle du texte à haute voix (10 min)

**M :** Sasa wanafunzi tatu wasome kwa sauti ya juu, mmoja Kiisha mwengine wasome kwa sauti ya cini, wakiweka kidole kwa kila kila neno wanasoma.

- Circuler et demander à 7 élèves de pointer les mots qui sont en train d'être lus.

#### Paka yetu

Nyumbani tunaishi na paka **pembeni**, jina lake ni Tomi. Mama na baba wamemubeba kila **jioni**. Wakati alikuwa mdogo, tulimulisha kwa maziwa.

Leo amewinda **panya** mwenyewe. Tomi hapendi maji lakini ni msafi. Amejiosha na **ulimi** wake. **Nyumbani**, tunapenda Tomi sisi wote.

### c. Compréhension du vocabulaire (5 minute)

**M :** Paka anaishi wapi kwa mtu ? **Pembeni**.

**M :** Pembeni ni karibu ya...

**M :** Sikilizeni msema yenye neno **Pembeni**: Nyumba yetu iko pembeni ya kiwanja ya ndege.

**M :** Sasa kila mmoja atunge msema yenye neno **Pembeni**.

- Suggérer des situations de communication, au besoin
- Faire de même avec **Ulimi na jioni**.

### d. Compréhension du texte (10 min)

**M :** Paka anaishi wapi ? (Pembeni ya mtu)

**M :** Paka anajiosha kwa nini ? (Kwa ulimi wake)

**M :** Sababu gani paka ana tabatia ya kulala kitini ao kitandani ? (kwani hapendi ucaf)

**M :** Namna gani umemuona Paka wenu ? (Réponse libre)

- Faire réfléchir en paire / banc, confronter les réponses et demander des justifications

## C. ACTIVITES DE CONTROLE

### 3. Evaluation (5 min)

#### a. Lecture des phrases du texte

- Choisir 7 à 10 élèves pour lire à haute voix des phrases du texte dans leur manuel. Noter et aider ceux qui ont des difficultés.

**M :** Someni kwa sauti ya juu misemwa ya usomi nita waonesha ndani ya vitabu vyenu.

#### b. Compréhension

**M :** Usomi wetu wa leo unasemea kuhusu nini ? (Paka yetu)

**M :** Sasa nitasema misemwa, kama ni kweli, inua kidole gumba, kama si kweli, tia mikono juu ya marfaa.

**M :** Paka huishi pembedi ya mtu)

**M :** Paka anajiosha kwa maji. (-)

**M :** Kitanda na kiti ndio nafasi paka analala ☝

**M :** Paka anaacha wazi ucaf wake (--)

**M :** Andika ndani ya buku yako majina mbalimbali inayo elekea nyama za ufugo.

#### Devoir à domicile

**M :** Wanafunzi wapenzi, nyumbani, musomee wazazi wenu usomi wa leo kwensiukurasa wa 47. Kiisha muandike misemwa zinazo elekea nyama za ufugo.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N° 12

### LEÇON N° 12.3

**Thème:** Les animaux

**Sous-thème :** les animaux domestiques

**Sujet de la leçon:** Paka yetu

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d'):

- relire avec expressivité le texte gradué
- identifier le complément du verbe dans une phrase (d'objet direct, indirect)
- Produire des phrases à l'oral et à l'écrit

**Matériel didactique:** Texte du Manuel de l'élève...

**Références:** Guide de l'enseignant ;  
Manuel de l'élève, p. 47-48

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Rappel des idées importantes du texte (5 min)

**M :** Usomi yetu ya jana ilisema kuhusu nini ? (Paka yetu).

**M :** Paka anaishi wapi? . (pembeni ya mtu)

**M :** Paka anajiosha kwa nini ?(kwa ulimi wake)

**M :** Sababu gani paka ana tabia ya kulala kitini ao kitandani? (kwani hapendi ucafu)

**M :** Wanani pia wanahitaji maji safi? (Samaki)

**M :** Namna gani umemuona paka wenu ?  
(Réponse libre)

- Choisir 2 à 3 élèves pour répondre à chaque question.

#### B. ACTIVITES PRINCIPALES

##### 2. Relecture du texte en paire à voix basse (15 min)

**M :** Mufungue vitabu vyenu kwa ukurasa wa 47.

**M :** Msome tena hadisi « **Paka yetu** » na mwenzako wa marfaa, mmoja kiisha mwengine. Mwenzako akimagumu, umusahihishe.

Wale wanaohitaji kusoma wainue mbele kidole.

**M :** Someni kwanza na sauti ya cini hadi mwisho. Mukibadilisha zamu, mmoja asome, na mwengine amusikilize.

- Circuler pour écouter les élèves lire et les aider au besoin.

- Après 2 minutes, demander aux autres de lire.

#### 3. Grammaire (20 min)

##### a. Appropriation des emplois de la règle: le complément du verbe (10 min)

**M :** Someni msemwa huu : **Paka anapenda usingizi**.

**M :** Sikilizeni namna ninavyo uliza kwa kupata neno "Usingizi"

**M :** Paka anapenda nini ? (**Usingizi**)

**M :** Neno **usingizi** ni nini ? **Timizo**. Basi timizo la tendo ni nini ?

« Timizo ni neno linalotimiza maana ya tendo. »

Kwa kupata « timizo » ndani ya msemwa, tunatumia ulizo « nani » ao « nini » nyuma ya tendo.

**M :** Someni tena msemwa huu: Mwili wake ni safi. Neno safi ni timizo la sura.

« Kuna aina mbalimbali zingine za timizo sawa vile : la tendo, la mahali, la wakati... »

- Penser à faire répéter.

##### b. Production de phrases avec le complément du verbe (10 min)

**M :** Kila mwanafunzi atunge misemwa munamo timizo la tendo, la sura ao la wakati. kiisha muiandike ndani ya buku zenu.

**M :** Wanafunzi wane wapite mbele waandike misemwa yao ku ubao.

- Interroger 2 à 3 élèves qui écrivent au tableau leur phrase. Faire appel aux autres élèves pour corriger.

#### C. ACTIVITES DE CONTROLE

##### 4. Evaluation (5 min)

**M :** Sasa, kila mmoja atunge misemwa mbili, na atie kistari cini ya timizo la tendo.

- Après 3 minutes, interroger 5 élèves pour qu'ils lisent leur propre phrase.

#### Devoir à Domicile

**M :** Nacagua ndani ya usomi, misemwa munamo timizo la tendo, la sura ao la wakati. kiisha muiandike ndani ya buku zenu,kwenyi ukurasa wa 48.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N°12

### LEÇON N° 12.4

**Thème:** Les animaux

**Sous-thème :** Les animaux domestiques

**Sujet de la leçon:** Les textes de la semaine

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d'):

- lire un texte gradué
- employer les mots de vocabulaire ciblés
- construire une phrase à l'oral et à l'écrit à partir d'une consigne

**Matériel didactique:** Image du manuel de l'élève...

**Références:** Guide de l'enseignant ;  
Manuel de l'élève, p. 47 et 49

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Consolidation (15 min)

**M :** Sasa, tutasoma hadisi yenyi tulijifunza wakati uliyopita

**M :** Fungueni vitabu vyenu kwenyi ukurasa wa 47. kiisha someni hadisi « Paka yetu » na sauti ya juu.

#### B. ACTIVITES PRINCIPALES

##### 2. Production orale (10 min)

###### a. Rappel du thème / sous-thème (5 min)

**M :** Juma hii mzima tulisemelea kuhusu nini ? (**Imbwaa na paka**)

**M :** Maneno gani mapya tulijifunza tokeya hadisi yetu kuhusu Imbwaa na paka.

###### b. Construction de phrases (5 min)

- Faire construire oralement des phrases ; le complément du verbe, faire poser la question pour trouver ce complément.

**M :** Mutunge msemwa ambao una “ timizo la tendo ”

**M :** Tunacagua msemwa : « Paka haitaji maji kwa kujiosha. »

**M :** Neno « **maji** » ni timizo la tendo.

**M :** Kila wakati mutapenda kutambua « timizo la tendo » Mtumiye ulizo « nani, nini, wapi, namna gani kiisha tendo »

- Ecrire au tableau les phrases intéressantes liées au thème que les élèves ont construites

#### 3. Production écrite (15 min)

- Donner une consigne et former des groupes de 4 élèves / 2 bancs

**M :** Sasa, Mtumike katika kundi ya wanafunzi wane wane kwa kila marfaa, muandike misemwa na mupike kistari cini la timizo la tendo.

**M :** Kwa kutambua mwenye timizo la tendo, mukumbuke ulizo : nani? nini? wapi? ao namna gani, kiisha tendo.

- Attendre 5 minutes et envoyer, au tableau, 3 élèves pour écrire leur phrase.

**M :** Sasa kiongozi wa kila kundi apite ku ubao aandike msemwa yenye waliandika katika kundi lao na kutia kistari cini ya timizo ya tendo.

**M :** Tazameni vizuri ginsi mwenzenu anaandika, kama anafanya makosa musahihishe.

#### C. ACTIVITES DE CONTROLE

##### 4. Evaluation (5 min)

**M :** Sasa, kila mmoja akamate buku yake aandike msemwa mbalimbali anayo kumbuku kuhusu tabia ya Paka

**M :** Kumbuku kuanza msemwa wako na : « Paka ... » Kiisha ongeza tendo na timizo lake.

#### Devoir à domicile

**M :** Wanafunzi wapenzi nyumbani muandike maneno tano kuhusu nyama za pori, kwenyi ukurasa wa 49. Kiisha misemwa mbili kwa kueleza kazi ya paka nyumbani.

#### Auto évaluation de l'enseignant:

Pour chaque activité dans cette leçon, comptez les élèves dans votre classe qui ont maîtrisé et pu faire cette activité. Si 50% ou plus de vos élèves n'ont pas pu faire une activité ou plusieurs des ACTIVITES, référez-vous au tableau « ACTIVITES de remédiation » à l'annexe de ce guide. Mener cette/ces activité(s) avec vos élèves avant d'avancer à la prochaine unité.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N° 13

### LEÇON N° 13.1

Thème : Les animaux

Sous-thème : Les animaux sauvages

**Sujet de la leçon:** Fisi, Tembo na Mbuluku

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d') :

- utiliser les mots du vocabulaire ciblés liés au thème
- répondre aux questions de compréhension du texte


**Matériel didactique:** Affiche n°13

**Références :** Guide de l'enseignant ;  
Manuel de l'élève, p. 50

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Observation et exploitation de l'image (10 min)

- Pointer l'image de l'affiche.



**M :** Tazameni vizuri sanamu hii,

**M :** Wawili wawili, wala kwa marfaa, kila mmoja aambie mwenzake ile anaona kwenyi sanamu.

**M :** Wanyama tatu hawa ni wanyama gani ?

**M :** Tembo iko inafanya nini?

**M :** Mbuluku nayo iko inafanya nini?

**M :** Kiisha ya kutazama sanamu izi, munazania hadisi yetu litasemea nini?

- Demander aux élèves de réfléchir par banc ; en choisir 2 à 3 pour répondre ; Apprécier les réponses différentes.

**M :** Sasa tutasoma, ili tuvumbue hadisi yetu inasema kuhusu nini.

#### B. ACTIVITES PRINCIPALES

##### 2. Etude du texte (25 min)

**Lecture du texte à haute voix (5 min)**

**M :** Mufwate hadisi hii vizuri. Kiisha mutajibu ku maulizo..

###### Fisi, tembo na mbuluku

Fisi alipokuwa akitembea **usiku**, alianguka shimi ni defu. Alipima kujiondosha umo lakini alipata magumu. Mapema, alianza kulalamika ili apate msaada.

Tembo aliposikia malalamiko hayo, alimuonea huruma, akasogea karibu ya tundu kwa kutazama. Fisi alipomuana akamuambia: « mjomba tembo, nina kusii unisaidie, nikamate mkia wako ili nitoke **shimoni** humo. Tembo akasema: unihapie hautanikula bahada ya kukutosha.

Fisi **alihapa** hata mtendea jambo mbovu lolote. Tembo akamuamini, akamuondoa shimi ni. Alipotoka shimi ni, Fisi akaanza kumuluma tembo kwa kumukula. Kwa bahati nzuri, mbuluku alikuwa akipita hapo. Aliwaomba **wajitetee**. Tembo akiweza kujiteya sababu ya uchungu ya vidonda. Fisi akaeleza uwongo.

Neno lenu ni ngumu asema mbuluku. Kila mmoja wenu arudi nafasi alikuwa ili **nielewe** na niwamuwe vizuri. Fisi akarudi shimi ni. Mbuluku akamuomba tembo aende zake na Fisi akabaki shimi ni.

##### b. Compréhension du vocabulaire (5 min)

**M :** Wakaki gani Fisi alitumbukia shimi ni defu ? (**Usiku**) ?

**M :** **Usiku** ni wakati wa giza. wakati watuwanalala.

**M :** Sikilizeni msemwa munamo neno **Usiku**. Mfano: **Usiku** watu wanalala.

**M :** Sasa nanyi vilevile mutunge misewa munamo neno “**usiku**.”

- Suggérer les situations de communication au besoin.  
➤ Faire la même chose avec les mots : Shimoni, Alihapa, wajiteteye.

##### c. Compréhension du texte (15 min)

- Relire le texte une fois et procéder par le questionnement par paire / banc.  
➤ Apprécier les réponses et demander des justifications.

**M :** Fwateni vizuri nitasoma tena hadisi yetu, badae, mutajibu ku maulizo.

**M :** wakati gani Fisi aliAanza kulalamika ? (Mapema)

**M :** Fisi alilalamika sababu gani ? (ili apate msaada)

**M :** Nani alimtosha Fisi shimonii ? (Tembo)

**M :** Kiisha ya Fisi kutoka shimonii alifanya nini ? (Akaanza kumuluma Tembo kwa kumukula)

**M :** Fisi alikosa nini kwa kutamani tena kumukula tembo aliyejemuaidia ? (Alikosa shukrani)

**M :** Sasa wewe adui wako akikuomba msaada utafanya nini ? (Reponse libre)

### C. ACTIVITES DE CONTROLE

#### 3. Evaluation (10 min)

##### a. Compréhension

**M :** Nitasema kuhusu hadisi yetu. Kama ni kweli, uinue kidole gumba. Kama msemwa si sawa, utie kidole juu ya marfaa.

**M :** Fisi aliAanza kulalamika mapema. ☺

**M :** Tembo alikataa kumtosha fisi shimonii. (--)

**M :** Kiisha kutoka shimonii fisi alimuluma Tembo. ☺

**M :** Fisi alikuwa na shukrani kwa tembo. (--)

**M :** Andika kwa misemwa mbili, andika matendo unafanya kusudi usiwe na adui.

##### b. Vocabulaire

**M :** Nitasema misemwa. Kama msemwa ni sawa, uinue kidole gumba. Kama msemwa si sawa, utie kidole juu ya marfaa.

**M :** Shimonii ni ndani ya shimo. ☺

**M :** Usiku ni wakati wakuceza (--)

**M :** Aliapa ni tendo kuapa, kuapa ni kuakikisha ☺

**M :** Kujiteteya ni kuliya (--)

#### Devoir à domicile

**M :** Wanafunzi wapenzi, nyumbani, muelezee wazazi na wandugu wenu hadisi ya leo. Kiisha muandike majina ya nyama za pori munazoona kunako sanamu , kwenyi ukurasa wa 50.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N° 13

### LEÇON N° 13.2

#### Thème: Les animaux

#### Sous-thème : Les animaux sauvages

**Sujet de la leçon:** Mamba na kima

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d'):

- lire avec expressivité le texte gradué
- employer les mots de vocabulaire ciblés
- répondre aux questions de compréhension sur le texte

**Matériel didactique:** Image du manuel de l'élève...

**Références:** Guide de l'enseignant ; Manuel de l'élève, p. 51

### A. ACTIVITES INITIALES

#### 1. Observation et exploitation de l'image (5 min)

**M :** Mufungue vitabu vyenu kwa ukurasa 51.

**M :** Tazameni sanamu hii.

**M :** Munaona nini ?

**M :** Mamba na Kima wanafanya nini?

**M :** Kutokea sanamu hii, munawazia hadisi ya leo itasemea nini?

- Demander aux élèves de réfléchir en paire / banc ; en choisir 3 à 4 pour répondre ; Apprécier les réponses différentes ; corriger et renforcer les réponses.



## B. ACTIVITÉS PRINCIPALES

### 2. Etude du texte (35 min)

#### a. Lecture du texte en paire à voix basse (10 min)

**M :** Tazameni usomi hii. Ina vipindi ngapi? Kipindi ya kwanza inaanza na neno gani, inaishia inaisha na neno gani?

**M :** Wawili wawili wala kwa marfaa, musome mmoja Kiisha mwengine. Anae magumu, mwenzake amusahihishe.

**M :** Yule atakaesoma wa kwanza ainue kidole na asome kwa sauti ya cini.

- Circuler pour écouter les élèves lire et les aider au besoin.
- Après 2 minutes, demander aux autres de lire

#### b. Lecture individuelle du texte à haute voix (10 min)

**M :** Sasa wanafunzi tatu wasome kwa sauti ya juu, mmoja Kiisha mwengine, na wale wanataka kusoma wasome kwa sauti ya cini, wakiweka kidole kwa kila neno wanasoma.

- Circuler et demander à 7 élèves de pointer les mots qui sont en train d'être lus.

#### Mamba na Kima

Mamba anaomba **kima** wawe marafiki. Tutaishi namna gani ? Ulizo la kima kwa mamba. Mimi nakaa mitini, nimejilisha kwa mbegu. Ila wewe umelala majini, nakujilisha kwa samaki.

Mamba akasema: tutaishi **mcana**, na kuacana usiku. Vema, inawezekana tuwe marafiki, kwa kuwa tunaishi porini. Mamba na kima wakawa **marafiki** wazuri.

#### c. Compréhension du vocabulaire (5 min)

**M :** Mamba aliomba nani wawe marafiki ? Kima.

**M :** Kima ni nyama pori inayo kaa juu ya mti.

**M :** Sikilizeni msema yenye neno Kima: Kima anatembeya mcana porini

**M :** Sasa kila mmoja atunge msema unayo neno Kima.

- Suggérer des situations de communication, au besoin
- Faire de même avec **Ulimi et anaflca**

#### d. Compréhension du texte (10 min)

**M :** Mamba aliomba kima wawe wa nani? (Marafiki)

**M :** Mamba anaishi wapi ? (Anaishi majini)

**M :** Sababu gani kwa mwanzo kima alishakia Rafiki wao ? (Kwani wanaishi nafasi mbalimbali)

**M :** Kwa mwisho waliamu nini ? (Kuwa marafiki)

**M :** Wewe rafiki yako ni nani ? (Réponse libre)

- Faire réfléchir en paire / banc, confronter les réponses et demander des justifications

## C. ACTIVITES DE CONTROLE

### 3. Evaluation (5 min)

#### a. Lecture des phrases du texte

- Choisir 7 à 10 élèves pour lire à haute voix des phrases du texte dans leur manuel. Noter et aider ceux qui ont des difficultés.

**M :** Someni kwa sauti ya juu misemwa ya Usomi nitakayo waonesha ndani ya vitabu vyenu.

#### b. Compréhension

**M :** Usomi wetu wa leo unasemea kuhusu nini ? (Urafiki wa mamba na kima)

**M :** Sasa nitasema misemwa, kama ni kweli, inua kidole gumba, kama si kweli, tia kidole juu ya marfaa.

**M :** Mamba aliomba kima wawe marafiki ➡

**M :** Kima alikubali kwa mara mojo (--)

**M :** Kwa mwisho walikubaliana kuwa marafiki ➡

**M :** Walikuwa wanalala pamoja (--)

**M :** Andika ndani ya buku yako jina yoyote inaelekea nyama ya pori.

#### Devoir à domicile

**M :** Nyumbani, Andika ndani ya buku yako msema kuhusu nyama za pori kwenyi ukurasa wa 51.

## UNITÉ D'APPRENTISSAGE N° 13

### LEÇON N° 13.3

#### Thème: Les animaux

#### Sous-thème : les animaux sauvages

**Sujet de la leçon:** Mamba na Kima

**Objectifs:** L'élève sera capable de (d'):

- relire avec expressivité le texte gradué
- identifier le complément du verbe dans une phrase (complément circonstanciel de lieu)
- Construire des phrases à l'oral et à l'écrit

**Matériel didactique:** Texte du Manuel de l'élève...

**Références:** Guide de l'enseignant ;  
Manuel de l'élève, p. 51-52

#### A. ACTIVITES INITIALES

##### 1. Rappel des idées importantes du texte (5 min)

**M :** Usomi yetu ya jana ilisema kuhusu nini ? (Mamba na Kima).

**M :** Mamba alimuomba kima wawe wa nani? (Marafiki)

**M :** Mamba anaishi wapi ? (Anaishi majini).

**M :** Sababu gani kwa mwanzo kima hakufurahia urafiki wao ? (Kwani wanaishi nafasi mbalimbali).

**M :** Kwa mwisho waliamua nini ? (Kuwa marafiki).

**M :** Wewe rafiki yako ni nani ? (Réponse libre).

